MFANO WA NOTISI YA FAINI YA MFUMO WA ASE

# NOTISI YA FAINI YA MFUMO WA KUTOZA FAINI KIOTOMATIKI KWA KUENDESHA GARI KWA KASI


Automated Enforcement Division
PO Box 593095
Orlando, FL 32839-3095

| | |
|---|---|
| Kiasi cha Kulipa: | $100 |
| Tarehe ya Kulipa: | |
| Nambari ya Kosa: | |

**Angalia na Ulipe katika:**
**www.ZeroFatality.com**
Namba Pleti:
Nenosiri:

Jina
Anwani
Jiji, Jimbo, Msimbo wa Eneo






Gari lako lilirekodiwa likiendeshwa kwa kasi, kinyume na vifungu vya sheria vya § 7-15-3 na § 8-1-2-6, ROA (1994), NMSA 1978 § 66-7-301 na NMSA 1978 § 66-7-104 vya Sheria ya Magari ya Jimbo la New Mexico.

Mahali:

Tarehe: Wakati:
Ishara ya kasi: Kasi:
Namba Pleti: Muundo wa Gari:

Kama mmiliki/mkodishaji wa gari aliyesajiliwa unawajibika kwa kosa hilo.

Faini ni kiasi cha $100.00 (maagizo ya malipo yanapatikana hapo chini). Hatua ya kulipa inachukuliwa kuwa kukubali na kuondoa haki yako ya kukata rufaa. Una siku thelathini kuanzia wakati wa kupokea notisi hii kulipa faini hiyo, kukata rufaa, kuwasilisha kiapo cha mmiliki au kuomba kutoa huduma kwa jamii. Usipolipa inaweza kusababisha kesi hii iripotiwe kwa kampuni ya ukusanyaji madeni.

KULIPA FAINI HAKUTASABABISHA KUONGEZEWA ALAMA KWA REKODI YAKO YA UDEREVA.

**Athari za kukosa kulipa na kuwa na zaidi ya deni moja la faini ya mfumo wa Kutoza Faini Kiotomatiki kwa Kuendesha Gari kwa Kasi (ASE, Automated Speed Enforcement):**

Ikiwa mmiliki aliyesajiliwa ana madeni mawili (2) au zaidi ya faini za mfumo wa ASE, mmiliki aliyesajiliwa anaweza kuchukuliwa hatua zinazoweza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na lakini si tu kuzuiwa kuegesha gari katika vituo vya maegesho, kuzuiwa kuendesha gari na/au kukamatwa kwa gari lake ikiwa gari lake litapatikana limeegeshwa kwenye barabara yoyote au kando ya barabara ndani ya Jiji la Albuquerque; kwenye au katika kituo chochote cha maegesho kinachomilikiwa na Jiji; kwenye au katika kituo chochote cha maegesho kinachosimamiwa na Jiji; au kwenye jengoi lolote linalomilikiwa na Jiji ndani ya vizuizi vya Jiji la Albuquerque (8-5-1-43 ROA 1994).

**Cheti cha Afisa wa Jiji la Albuquerque**
Kulingana na uchunguzi binafsi wa picha za gari zinazoonyesha ukiukaji wa vifungu vya sheria vya § 7-15-3 na § 8-1-2-6, ROA (1994), NMSA 1978 § 66-7-301 na NMSA 1978 § 66-7-104 vya Sheria ya Magari ya Jimbo la New Mexico.

Imeapwa kwa au imethibitishwa na:

__________________________
Saini ya Idara ya Polisi

Bandua hapa na urudishe na malipo yako

## LIPA MTANDAONI

Unaweza kuona kosa lako na kulipa faini yako ukitumia namba pleti na nenosiri lako hapa chini.

**Tovuti ya Malipo:** ZeroFatality.com
**Namba pleti:**
**Nenosiri:**

## LIPA NA SIMU

Tafadhali piga simu kwa Kitengo cha Kutoza Faini Kiotomatiki kwa Kuendesha Gari kwa Kasi (Automated Enforcement Division), bila malipo wakati wowote, usiku na mchana, kila siku: (Wahudumu wanapatikana: Jumatatu hadi Ijumaa, Saa nne asubuhi (10 AM) hadi saa kumi na moja jioni (5 PM) (ET))

**Nambari ya simu:** (866) 247-8157
**Nambari ya Kosa:**
**Nambari ya Siri:**

**Kiasi cha Kulipa: $100**
**Tarehe ya Kulipa:**

## LIPA KWA BARUA

**Cheki au Hawala ya Fedha (Money Order), Inayoweza kulipwa kwa:**

**PO Box 593095, Orlando, FL 32859-3095**

**Tafadhali ambatisha stakabadhi hii na malipo yako**

**USITUME PESA KWA BARUA**

## LIPA MWENYEWE

**mated Enforcement Division**
**ivic Plaza, Basement Room B2090**
**Albuquerque,NM 87102**
Mon – Fri: 8:00 AM – 5:00 PM(MT)
Cheki ya Kulipwa kwa Keshia, Hawala ya Fedha (Money Order) au Pesa Taslimu
Beba nakala ya cheti cha kosa au nambari ya kosa na namba pleti.

## TAFSIRI YA KOSA

Español-Tiếng Việt-简体中文- العربية العربى
Espalugha ya kiswahili

Tembelea: www.cabq.gov/ase

TAFADHALI KUMBUKA: Ada ya huduma ya $6.95 itaongezwa kwa malipo yote ya simu na ya mtandaoni.
Tafadhali bofya kitufe cha malipo mara moja pekee. USIFANYE jaribio la pili la kulipa kwa siku moja.

# MFANO WA NOTISI YA FAINI YA MFUMO WA ASE

# Kuendeleza, Kulinda na Kuboresha Afya, Usalama na Ustawi wa Raia Wetu

**www.ZeroFatality.com**

## NINAWEZAJE KULIPA FAINI YANGU?

- **LIPA MTANDAONI:** Tafadhali tembelea www.ZeroFatality.com
- **LIPA NA SIMU:** Tafadhali wasiliana na Kituo cha Mawasiliano ya Huduma kwa Wateja (Customer Service Call Center) bila malipo kwa nambari (866) 247-8157 ili ulipe na kadi ya mikopo/benki au ACH wakati wowote, usiku na mchana, kila wakati. Kati ya saa mbili asubuhi (8:00 AM) na saa tisa alasiri (3:00 PM) (MT), Jumatatu hadi Ijumaa, mhudumu atakusaidia kulipa na kadi ya mikopo/benki au ACH.
- **LIPA MWENYEWE:** Tafadhali beba nakala ya cheti cha kosa au nambari ya kosa na namba pleti:
  Jumatatu hadi Ijumaa: Saa mbili asubuhi (8:00 AM) hadi saa kumi na moja jioni (5:00 PM) (MT)
  **Njia za malipo ya kulipa mwenyewe Zinazoruhusiwa pekee: Cheki ya Kulipa kwa Keshia, Hawala ya Fedha (Money Order) au Pesa Taslimu**
- ***LIPA KWA BARUA****: Ili ulipe faini ya Kosa, tuma stakabdhi ya malipo pamoja na cheki au hawala ya fedha (money order) (SI PESA TASLIMU) inayoweza kulipwa kwa. Ili uhakikishe malipo yanafanywa ipasavyo, chapisha Nambari ya Kosa na namba pleti yako kwenye malipo yako. Tafadhali ruhusu siku 5 za kuwasilishwa.*

***Tuma malipo kwa:***

**AUTOMATED ENFORCEMENT DIVISION**
P.O. Box 593095
Orlando, FL 32859-3095

TAFADHALI KUMBUKA: Ada ya huduma ya $6.95 itaongezwa kwa malipo yote ya simu na ya mtandaoni.

## ITAKUWAJE IKIWA SI MIMI NILIYEKUWA NINAENDESHA GARI LANGU WAKATI WA KUFANYIKA KWA KOSA?

Unaweza kuwasilisha Kiapo cha Mmiliki (Owner's Affidavit) kinachomtambulisha dereva anayehusika ili Notisi ya Faini ya Mfumo wa Kutoza Faini Kiotomatiki kwa Kuendesha Gari kwa Kasi (ASE, Automated Speed Enforcement System) iweze kutumwa kwa dereva huyo. Kiapo cha Mmiliki (Owner's Affidavit) lazima kithibitishwe rasmi. Mmiliki aliyesajiliwa anayepokea notisi ya kwanza ya faina ya mfumo ndiye tu anayeweza kuwasilisha kiapo cha mmiliki kinachompendekeza mtu mwingine. Mtu aliyependekezwa hapaswi kumpendekeza mtu mwingine kama dereva. Hakuna mtu mwingine anayeruhusiwa kupendekezwa. Njia ya pekee ya mtu aliyependekezwa ya kupinga kosa husika ni kuomba kukata rufaa haraka iwezekanavyo. (angalia hapa chini) Utapata anwani ya kutuma barua katika sehemu ya chini ya fomu ya Kiapo cha Mmiliki (Owner's Affidavit) na unaweza kupata fomu hiyo mtandaoni katika: www.ZeroFatality.com

## JE, KUNA PINGAMIZI NYINGINE ZOZOTE SAHIHI KWA NOTISI HII YA FAINI YA MFUMO?

Ndiyo. Ili kupinga kosa hili, unaweza kuomba kukata rufaa kabla ya tarehe ya mwisho iliyowekwa kwenye Notisi yako. Usipoomba kukata rufaa kufikia tarehe ya mwisho iliyowekwa kwenye Notisi yako utapoteza haki ya kukata rufaa. Ikiwa kosa halifutwa baada ya kesi yako, **lazima ulipe faini yako.**

Kuwasilisha kiapo cha uongo ni kosa la daraja la nne, linaloweza kuadhibiwa katika Jimbo la New Mexico. § 30-25-1.

## UNA HAKI YA KUANGALIA PICHA KWA MBALI:

Una haki ya kuangalia video au picha za kielektroniki mtandaoni katika:
www.ZeroFatality.com

## ITAKUWAJE IKIWA SITALIPA FAINI?

Usipolipa faini yako au kuipinga kufikia tarehe ya mwisho, au usipokamilisha saa 4 za kutoa huduma kwa jamii ndani ya siku 90, au uamuzi wa Kiapo cha Mmiliki au kesi yako usipokupendelea, utawajibika kulipa faini ya kiasi cha $100. Usipolipa kiasi chote unachopaswa kulipa, deni lako linaweza kuripotiwa kwa shirika la ukusanyaji madeni, au Jiji linaweza kutafuta njia nyingine zote za kukusanya deni hilo.

## JE, UNA MASWALI?

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu Kosa hili, tafadhali wasiliana na Kituo cha Mawasiliano ya Huduma kwa Wateja cha Kitengo cha Kutoza Faini Kiotomatiki cha Albuquerque (Albuquerque Automated Enforcement Division Customer Service Call Center) bila malipo kwa nambari 866-247-8157 kati ya saa mbili asubuhi (8:00 AM) na saa tisa alasiri (3:00 PM) (MT). Au piga simu kwa nambari 311
Jumatatu hadi Ijumaa.

## HUFANYAJE KAZI?

Mfumo wa kutoza faini kwa kurekodi picha hupima kasi na nafasi kwa kutumia rada ya ufuatiliaji mwingi. Ikiwa unapitisha kikomo cha kasi kilichoonyeshwa, hurekodi picha za kidijitali za gari lako. Mfumo huo pia hurekodi video ya mwendo unayoweza kuiona mtandaoni. Idara ya Polisi ya Albuquerque (Albuquerque Police Department) hukagua kila kosa mahususi.

## NINAWEZAJE KUPINGA NOTISI YA KOSA?

Unaweza kuomba kukata rufaa kabla ya tarehe ya mwisho iliyowekwa kwenye Notisi yako. Utapata fomu ya kuomba kukata rufaa mtandaoni katika: www.ZeroFatality.com. Katika kesi yako: Kanuni za ushahidi za jimbo la New Mexico, Kanuni za Kesi ya Kiraia za jimbo la New Mexico na Amri za Ofisi Huru ya Maamuzi ya Kesi ya Albuquerque (Albuquerque Independent Office of Hearings Ordinances) zitatumika.

## NINAWEZA KUTOA HUDUMA KWA JAMII BADALA YA KULIPA FAINI?

Ndiyo, unaweza kuchagua kutoa huduma kwa jamii kwa saa 4 badala ya kulipa faini ya kiasi cha $100. Lazima ueleze nia yako ya kutoa huduma kwa jamii kufikia tarehe ya mwisho iliyowekwa kwenye Notisi, ambayo ni siku 30 kuanzia tarehe ya kupokea notisi ya faini ya mfumo. Tafadhali kumbuka kwamba lazima ukamilishe saa 4 za kutoa huduma kwa jamii ndani ya siku 90 baada ya kupokea notisi ya faini ya mfumo, ili deni lako lizingatiwe kuwa limelipwa kikamilifu. Ikiwa ungependa kutumia fursa hii kulipa jamii na muda wako, kwa maelezo zaidi nenda katika:www.ZeroFatality.com

## Athari za kukosa kulipa na kuwa na zaidi ya deni moja la faini ya mfumo wa Kutoza Faini Kiotomatiki kwa Kuendesha Gari kwa Kasi (ASE, Automated Speed Enforcement)

Ikiwa mmiliki aliyesajiliwa ana madeni mawili (2) au zaidi ya faini za mfumo wa ASE, mmiliki aliyesajiliwa anaweza kuchukuliwa hatua zinazoweza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na lakini si tu kuzuiwa kuegesha gari katika vituo vya maegesho, kuzuiwa kuendesha gari na/au kukamatwa kwa gari lake ikiwa gari lake litapatikana limeegeshwa kwenye barabara yoyote au kando ya barabara ndani ya Jiji la Albuquerque; kwenye au katika kituo chochote cha maegesho kinachomilikiwa na Jiji; kwenye au katika kituo chochote cha maegesho kinachosimamiwa na Jiji; au kwenye jengoi lolote linalomilikiwa na Jiji ndani ya vizuizi vya Jiji la Albuquerque (8-5-1-43 ROA 1994).

***Mail To:*** Automated Enforcement Division
PO Box 593095
Orlando, FL 32859-3095

SAMPLE ASE SYSTEM FINE NOTICE